# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS - TAMISEMI
# HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA-MIKINDANI
# SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MTWARA

S. L. P 164,

MTWARA.

**10/05/2018**

**NAMBA ZA SIMU**

Mkuu wa Shule: - 0754-416485 au 0785-233324
Makamu Mkuu wa Shule: - 0713-743270 au 0786-730333
Mwalimu wa Malezi (Matron): - 0658-842724 au 0788-636152

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi; ..............................................................................

S. L. P ..................................

..................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MTWARA 2018/19.**

Hongera!

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na KIDATO CHA TANO (V) katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mtwara. Anatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe 01/07/2018 akichelewa wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua shule atakuwa amepoteza nafasi yake na itachukuliwa na mtu mwingine kama ilivyotangazwa.

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule hii ni ya Bweni na ipo umbali wa kilomita saba (7) kusini mwa Mji Mkuu wa Mkoa na Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Usafiri wa Daladala kutoka katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mtwara unapatikana. Kufika shuleni tumia Daladala za SOKO KUU-NALIENDELE na shuka kituo cha MANGAMBA (KIBAONI) utaona kibao cha shule.

**ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE.**

**(A) ADA**

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= ambayo inalipwa kupitia Benki ya NMB katika ACCOUNT Na. 70601200072 ya Mtwara Girls Secondary School. Aidha unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula au Shilingi 70,000/= kwa mwaka mmoja wa masomo. Andika kwenye risiti ya benki (Bank Pay In Slip) jina la Mwanafunzi.

**(B) MICHANGO MBALIMBALI**

1) 10,000/= Kwa ajili ya Afya (Huduma ya kwanza)
2) 6,000/= Kwa ajili ya kitambulisho.
3) 5,000/= Tahadhari.
4) 20,000/= Kwa ajili ya Taaluma.
5) 30,000/= Kwa ajili ya kuwalipa vibarua (Wapishi, Walinzi n,k).
6) 15,000/= Mchango wa ukarabati wa samani.
7) 20,000/= Mitihani ya kujipima (Mock)
8) 2,000/= Nembo ya shule.

**JUMLA YA MICHANGO MBALIMBALI;**

Jumla ya michango mbalimbali ya shule ni Tshs 108,000/= ambayo inatakiwa iingizwe kwenye Benki ya NBC Akaunti Na. 034103002085, Jina la akaunti Mtwara Girls Secondary School. Pia uje na risiti halisi (Original) ya benki (Bank Pay In Slip) iliyoandikwa jina la mwanafunzi.

**NB**: i. Fedha za matibabu zitatumika kununua dawa muhimu. Gharama hizi hazihusishi matibabu nje ya shule.

ii. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa na Nakala ya Matokeo (Results slip) ya kidato cha nne.

iii. Nguo za ndani za kutosha na vifaa vya usafi (Pedi)

**(C) VIFAA MUHIMU AMBAVYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.**

1) Rimu moja ya Karatasi (A4).
2) Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika.
3) Dissecting kit kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.
4) Scientific Calculator kwa wanafunzi wa EGM, HGE na CBG.
5) Godoro ft 2.5 x 6 7) Shuka Jozi mbili rangi ya Bluu bahari.
6) Chandarua
7) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuri, kijiko na kikombe)
8) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
9) Fyekeo moja (1)
10) Jembe moja (1) lenye mpini.
11) Fagio la kusukumia maji (Rubber Squeezer) moja (1)
12) Fagio laini (Soft broom) moja (1)
13) Fagio ngumu (Hard broom) moja (1)
14) Fagio la chelewa moja (1)
15) Track Suit moja (1) ya michezo rangi ya Bluu mpauko (Light blue)
16) Raba za michezo.
17) Sanduku Imara la kutunzia vifaa vyake (Tranka).
18) Tochi ya kumsaidia wakati umeme ukikatika.
19) Dawa ya kusafishia choo Lita Tano (5).

**NB**; Vifaa kama Rimu, Scientific Calculator, Godoro, Vyombo vya chakula, Jembe, Ndoo, Fyekeo, Fagio zote, Dawa za kusafishia choo pia vinauzwa shuleni kuepusha usumbufu wa mizigo njiani.

**(D) SARE ZA SHULE:**

A. Mashati mawili meupe mikono mifupi yenye ukubwa wa kutosha bila kuchomoka likichomekewa au Nusu kanzu ndefu nyeupe mbili (na isibane kwa kuonyesha umbile) kwa wanaovaa hijabu.

B. Sketi mbili (2) kitambaa cha Kotoni Mzito (Nyekundu) mshono wa linda boxi NDEFU hadi mwisho wa ugoko wa mguu

C. Magauni mawili MAREFU hadi mwisho wa goko za miguu za kushindia (Shamba Dress) rangi ya Damu ya Mzee kitambaa cha Kotoni Mzito mshono wa Linda Boksi.

D. Mitandio miwili (2) ya Rangi ya pinki (kawida isiyo na maua) ya kujistiri baada ya muda wa vipindi (Kwa waislamu)

E. Majuba mawili (2) ya Rangi ya Pinki (Kawaida yasiyo na maua) ya kujisitiri baada ya muda wa vipindi (Kwa waislamu)

F. Hijabu ndefu nyeusi kwa ajili ya kuendea msikitini tu kwa waislamu wanaoswali.

G. Viatu vyeupe (Raba za kamba) vya kufunika miguu visivyo na visigino virefu (jozi mbili).

H. Soksi nyeupe ndefu (jozi mbili).

I. Sweater (Rangi ya Bluu nyeusi/Dark blue) kwa ajili ya kipindi kifupi cha baridi wakati wa darasani.

**N.B; MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUSUKA NYWELE AU KUFUGA NYWELE NDEFU.**

**SHERIA ZA SHULE**

1. Wanafunzi wasimame na kusalimia mwalimu au mtu yeyote anayewazidi umri anapopita au anapoingia darasani au kwenye Ukumbi wa mikutano.
2. Wanafunzi wampokee mzigo mwalimu au mtu anayewazidi umri pindi anapopita karibu yao.
3. Wanafunzi waheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wao.
4. Ni mwiko mwanafunzi kutumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao, kwa walimu, watumishi wasiowalimu, au viongozi wa serikali ya wanafunzi na watuwengine.
5. Wanafunzi waheshimiane na kusaidiana wao kwa wao . Ni marufuku kwa wakubwa kuwanyanyasa wadogo.
6. Wanafunzi wapende kujituma na kuheshimu kazi za aina zote.
7. Wanafunzi watii kengele ya shule pindi inapogonwa kwa kukimbilia eneo husika.
8. Wanafunzi waheshimu Bendera ya Taifa, Viongozi wa Serikali, Wimbo wa Taifa na Bendera ya Taifa pindi inapopandishwa na kushushwa.
9. Ni mwiko kwa wanafunzi kufanya mambo yafuatayo:-
    - a) Kufuga kucha ndefu
    - b) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima na yanayoonyesha mabega.
    - c) Kupigana
    - d) Kuongeza mapambo juu ya sare ya shule kama vile:- (Kuvaa bangili, heleni, shanga, mkanda n.k)
    - e) Kupaka rangi ya kucha na macho (Wanja)
    - f) Kukata nyusi
    - g) Kutia dawa nywele mfano; Reluxer, Curls.
    - h) Kukata nywele Panki. i) Kusuka nywele.
    - j) Kukaribisha au kupokea wageni nje ya utaratibu wa shule.
10. Wanafunzi waheshimu Ofisi zote za shule.
11. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo:-
    - a) Jiko la Shule mpaka anapokuwa mwanafunzi wa zamu au kwa ruhusa maalumu.
    - b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wengine mpaka kwa kibali cha mkuu wa shule.
    - c) Nyumba za kufikia wageni (GUEST HOUSE).
    - d) Vilabu vya pombe.
    - e) Majumba ya starehe.
12. Wanafunzi waonyeshe heshima wanapokuwa kwenye ukumbi wa mikutano na chakula.
13. Wawapo darasani wanyooshe mikono juu na wasimame wanapojibu na kuuliza maswali
14. Wanafunzi wahudhurie vipindi vyote vya Darasani na kazi za mikono pindi zinapotolewa
15. Wanafunzi wafanye bidii katika masomo. Ni mwiko kupata alama chini ya 50% (Asilimia Hamsini) katika somo lolote.
16. Wanafunzi wahudhurie mikutano yote ya shule kama vile; Baraza la shule, Kupandisha bendera ya Taifa, Mikutano ya darasani na bweni.
17. Wanafunzi waendapo likizo lazima warudi shuleni kwa tarehe zilizopangwa.
18. Wanafunzi wavae sare ya shule wakati wote wa:-
    - a) Masomo darasani
    - b) Kusafiri kwenda likizo au kurudi shuleni
    - c) Safari za shule
    - d) Kwenda Hospitali
    - e) Mhadhara wa shule ikiwa ni pamoja na Baraza la shule
19. Wanafunzi wasitoke nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE**

a) Wizi

b) Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule

c) Utoro

d) Ulevi wa aina yeyote na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k

e) Uasherati, uhusiono wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

f) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

h) Kutaka kujiua

i) Kutokuwepo shuleni kwa muda wa miezi mitatu mfululizo bila taarifa

j) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

k) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.

l) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

m) Kudharau Bendera ya Taifa

n) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, waalimu/walezi na jamii kwa ujumla.

o) Kusuka au kufuga nyele ndefu.

p) Kufuga ndevu.

q) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.

r) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (GUEST HOUSE)

**TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI**

(Form hii ijazwe na irudishwe shuleni)

1. Jina la mwanafunzi ............................................................................ Kidato cha...............................
2. Kabila la mwanafunzi ..........................................................................................................................
3. (a) Tarehe ya kuzaliwa; ......................................................................................................................
   (b) Wilaya alikozaliwa mwanafunzi; ....................................................................................................
   (c) Mkoa; ..............................................................................................................................................
4. Dini ya mwanafunzi; ............................................................................................................................
5. Tatizo la mwanafunzi kiafya; ...............................................................................................................
6. Tatizo la mwanafunzi kitabia; ..............................................................................................................
7. Jina kamili la baba; ..............................................................................................................................
   Anuani kamili: ................................................................... Simu .......................................................
   Kazi yake: ...........................................................................................................................................
8. Jina kamili la mama; ...........................................................................................................................
   Anuani kamili: ............................................................. Simu .............................................................
   Kazi yake: ...........................................................................................................................................
9. Jina kamili la mtu/mlezi anayemhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake muhimu;
.............................................................................................................................................................
10. Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi; ...................................................................................................
    Anuani kamili; ................................................................. Simu ........................................................
    Kazi yake; ....................................................................Umri .......................................................
11. Orodha ya ndugu aliozaliwanao mwanafunzi, wakianza na wakwanza kuzaliwa;

| NA | JINA | UMRI | KAZI/MWANAFUNZI | KITUO CHA KAZI/SHULE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

12. Baba na mama wanaishi pamoja / wametengana (kata isiyohusika)

13. Uwepo wa wazazi: Baba - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini ..................................................
    Mama - YUPO/HAYUPO kama amefariki lini .................................................

14. Majina na picha za watu wasiozidi watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi;-

| **PICHA** | **PICHA** | **PICHA** |
|---|---|---|
| JINA | JINA | JINA |
| SIMU | SIMU | SIMU |
| UHUSIANO | UHUSIANO | UHUSIANO |

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi .................................................................... ambaye ni mzazi wa ...................................................

aliyetoka shule ya ......................................................Wilayani ...................................Mkoa wa................

nimesoma na nimeyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na ninaahidi kuwa nitajitahidi kumpatia mahitaji muhimu binti yangu aliyetajwa hapo juu hadi atakapomaliza ELIMU YA SEKONDARI

Sahihi .................................................................... Tarehe ......................................................................

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ......................................................................................... wa kidato cha .....................................

Nimesoma na kuzielewa sheria za shule, na naahidi kuzitii na kutimiza taratibu zote zilizowekwa.

Sahihi .................................................................... Tarehe ..................................................................

---

**Anangisye, S**

**MKUU WA SHULE**

**MTWARA - MIKINDANI MUNICIPAL COUNCIL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

THE HEADMISTRESS,
MTWARA GIRLS SEC/SCHOOL,
P. O. BOX 164,
**MTWARA.**

DATE: ..................................

TO:
The Medical Officer
.................................................
.................................................
……………………………………

**RE: NAME ...........................................................................................................................**

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary Education at Mtwara Girls Secondary School.

1. Eye sight ....................................................................................................................
2. Hearing ......................................................................................................................
3. Speech .......................................................................................................................
4. Venereal Diseases ......................................................................................................
5. Neurosis .....................................................................................................................
6. Pregnancy ..................................................................................................................

Doctor's Remarks .................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
Doctor's Advice ....................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................

Doctor's Name ......................................................................................................................
Signature ............................................... Rubber Stamp ……………………………………..
Date .......................................................................................................................................